**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

# BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI

## TAARIFA KWA UMMA

### KUSITISHA MATUMIZI YA NeST KWA MAAFISA UNUNUZI NA UGAVI WASIOKUWA NA USAJILI WA PSPTB.

**Dodoma 17, Julai, 2025.**

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) inawataarifu maafisa wote wa ununuzi na ugavi kuwa mfumo wa usajili wa PSPTB kwa njia ya mtandao (ORS) na mfumo wa ununuzi wa kielekroniki wa Tanzania (NeST) imefungamanishwa katika utekelezaji majukumu yao kwa njia ya kielekroniki.

Kutokana na kufungamanishwa huko, PSPTB inawataarifu maafisa wote wa ununuzi na ugavi wanaotekeleza majukumu yao kwa kutumia mfumo wa NeST bila usajili wa PSPTB hawataweza kutekeleza majukumu hayo ifikapo tarehe 31 Disemba, 2025.

Hivyo, PSPTB inatoa rai kwa maafisa hao kuhakikisha wamepata usajili wa PSPTB kabla ya tarehe tajwa ili waweze kuwa na sifa za kitaaluma na kuweza kutekeleza majukumu yao kupitia mfumo wa NeST.

**Imetolewa na:**

Digitally Signed By Godfred B. Mbanyi
Mon Jul 21 11:38:26 EAT 2025

Godfred B. Mbanyi
**MKURUGENZI MTENDAJI**

*Mkandarasi Place, Ghorofa ya 7, S.L.P. 2663, Dodoma. Simu: +255 22 2865860 Nukushi: +255 22 2862138. Tovuti: http://www.psptb.go.tz.*
*Barua pepe: barua@psptb.go.tz*